**LEARNING BY EAR - “Girls’ Rights”**

**EPISODE 9:**

**Title: “Girls' sexuality” – A Story of Girls’ Rights**

**AUTHOR**: **Njoki Muhoho**

**EDITORS: Andrea Schmidt, Katrin Ogunsade**

**Proofreading: Michael Lawton**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

**Characters:**

**SCENE 1 SCHOOL PLAYING GROUND**

| | | |
|---|---|---|
| Narrator | - | 30s Male |
| Ciro | - | 14 Female |
| Cheptoo | - | 15 Female |
| Fatuma | | -14 Female |

**SCENE 2 - VILLAGE PATH**

| | | |
|---|---|---|
| Ciro | - | 14 Female |
| Cheptoo | - | 15 Female |

**SCENE 3 - PLAYING FIELDS – GIRLS’ PARLIAMENT**

| | | |
|---|---|---|
| Ciro | - | 14 Female |
| Cheptoo | - | 15 Female |
| Fatuma | | -14 Female |
| 3-4 girls | | (13-16) |

**SCENE 4 - CIRO’S CLASSROOM. LUNCH HOUR**

| | | |
|---|---|---|
| Ciro | - | 14 Female |
| Cheptoo | - | 15 Female |
| Narrator | - | 30s Male |
| Fatuma | | - 14 Female |

**SCENE 5 - GIRLS’ PARLIAMENT**

| | | |
|---|---|---|
| Ciro | - | 14 Female |
| Cheptoo | - | 15 Female |
| Narrator | - | 30s Male |

| | | |
|---|---|---|
| Fatuma | - | 14 Female |
| Teacher Mona - | | 35 Female |
| Janet-Social Worker | | -30s Female |
| 5-6 girls (song!) | | (13-16) |

**01. INTRO**

**02. MUSIC: THEME MUSIC**

03. **NARRATOR**

Hujambo na karibu kwa makala nyingine kwenye msururu huu wa vipindi vya Learning By Ear, Noa Bongo Jenga maisha yako tukiwa bado kwenye mchezo kuhusu suala la **Haki za wasichana**. Katika kipindi kilichotangulia Wasichana wakumbwa na changamoto za uongozi. Hata hivyo lakini, kwa kuzingatia zaidi vigezo vya uongozi bora badala ya ubaguzi wa jinsia katika kampeini zake, Cheptoo achaguliwa kuwa kinara mkuu wa shule yao.

Na katika kipindi cha leo Ciro, Cheptoo na Fatuma wanajadilia hoja kuhusu uhusiano wa ngono. Tuungane na wasichana hawa wanapojadilia hoja hii.

**SCENE 1: SCHOOL PLAY GROUND**

**04. SFX: PLAY GROUND NOISES**

| | | |
|---|---|---|
| 05. | **CHEPTOO** | Ciro…., Fatuma yule…! Nadhani anakuja upande huu.. Fatu.. Fatu… tuko hapa |
| 06. | **CIRO** | Fatuma.. Kwanini umebadilisha mtindo wa kutembea? |
| 07. | **FATUMA** | (GRUDGINGLY) Mbona mtindo huu wa kutembea? Watushangaza! |
| 08. | **CHEPTOO** | Tembea vizuri! Waonea nini haya sasa..? Au ni kwasababu ya matiti yako? |
| **09.** | **CIRO** | Matiti yake yameanza kuwa makubwa na naona ameanza kujihisi msichana mkubwa sasa,..! ndio sababu.. hebu mtazame.. mtazama**…!** |
| 10. | **FATUMA** | Niacheni mie …Niacehni.. |
| 11. | **CHEPTOO** | Fatuma, huenda umenipita kwa umri, lakini nakwambia hivi, msichana kutoa matiti ni jambo la kawaida. Fatuma hili ni jambo la kawaida. Ndio daraja la kuvuka na kuingia Utu uzima.Usione haya.! Lazima ujiamini kama mwanamke. |

| | | |
|---|---|---|
| 12. | **CIRO** | Ndio , Unapaswa kujivunia kuwa Mwanamke! .Hebu nitazame mimi!.Fatuma  mabega yako yarudishe nyuma na kifua,kidevu mbele. |
| 13. | **FATUMA** | Ooh  mwenzangu….! Wavulana hunitania na kunifanya niona haya. |
| 14. | **CHEPTOO** | Wanakutania?. Wafahamu kwamba hili ni jambo la kawaida maishani. Lazima sote tufahamu vyema mili yetu, au sivyo? |

**15. <u>BRIDGE MUSIC</u>**

**<u>SCENE 2  VILLAGE PATH</u>**

**16. <u>SFX: FARM NOISES; FOOTSTEPS</u>**

| | | |
|---|---|---|
| 17. | **CIRO** | Cheptoo, Nashangaa kwani nini umeamua kunisindikiza nyumbani. Wewe kwenu ni upande ule na kwetu ni upande huu mwengine. |
| 18. | **CHEPTOO** | Ciro,si unanifahamu vyema sababu yenyewe. Kuna kitu nataka tuzungumze. |
| 19. | **CIRO** | Nini? |
| 20. | **CHEPTOO** | Usijali.. unajua ..  si rahisi….. |

| | | |
|---|---|---|
| 21. | **CIRO** | (LAUGHING) Cheptoo sikudhania kwamba mambo haya yanaweza kukutatiza. |
| 22. | **CHEPTOO** | Ni kweli… lakini … ni binamu yako Abdi! |
| 23. | **CIRO** | Binamu yangu mtukutu amefanya nini tena…? |
| 24. | **CHEPTOO** | Mimi .. mimi… ahh sawa tu…. Si mbaya viiiiiile!. |
| 25. | **CIRO** | (SHOCKED) Sikuamini ..! kwani unampenda..? yaani vita vyote hivyo ilikuwa ni kujifanya tu. |
| 26. | **CHEPTOO** | Shhhh usizungumze kwa sauti. Tumekuwa tukiongea…. Mara nyingi! |
| 27. | **CIRO** | Ehhheee, unamtongoza binamu yangu na hujaniambia…! lakini sawa nyote nyinyi ni watoto. |
| 28. | **CHEPTOO** | Sote ni wakubwa sasa, tumetimu miaka 15.. unanjua … unajua ni jambo la kawaida lakini…. ni kama tunapendana!. |
| 29. | **CIRO** | Unanishangaza. Wewe na Abdi?. Hilo ndilo ulitaka kuniambia? |
| 30. | **CHEPTOO** | Kuna zaidi…! |

31. **CIRO** Endelea nakusikiliza.

32. **CHEPTOO** Anataka tu… tuuuu ….

33. **CIRO** Kufanya nini (SILENCE) Unamaanisha… ku…ku . kufanya mapenzi?

34. **CHEPTOO** Shshhhhh..Nimekwambia usiongee kwa sauti. Jambo hili lanitatiza. Sijui nifanyeje .. unafikiri tunaweza kufanya…

35. **CIRO** Sijui, Cheptoo. Lakini sioni kama hiyo ni sawa. Uko tayari kufanya mambo haya? Lakini, lisikutatize, tunaweza kuitisha kikao cha bunge kulijadili suala hili?.

36. **CHEPTOO** Twende katika mkao wa bunge la wasichana.Lakini safari hii ni wasichana pekee!

**37. <u>BRIDGE MUSIC</u>**

**<u>SCENE 3 PLAYING FIELDS</u>**

**38. SOUNDS: PLAYGROUND NOISES, GIRLS CHATTERING AND LAUGHING (studio)**

39. **CHEPTOO** Nawashukuru nyote kwa kutenga muda wenu wa mapumziko baada ya masomo kuhudhuria kikao hiki cha dharura cha bunge la wasichana.

| | | |
|---|---|---|
| 40. | **CIRO** | Hapa kuna mjadala mpya uliowasilishwa. Na unahusu hali ya mili yetu na uhusiano wa kimapenzi …yaani .. yale mambo ambayo mara nyingi tunashindwa kuyazungumzia hadharani hasa kwa watu waliombele zetu. |
| 41. | **CHEPTOO** | Kama ngono! |
| 42. | **FATUMA** | ssshhhh , Cheptoo,kwani ni lazima usema wazi wazi na sauti ya juu. |
| 43. | **CHEPTOO** | Hii ndio hoja tunayojadilia hapa. Sasa mwaona, hata mnaogopa kutamka neno lenyewe pasi na kuangalia nani yuko nyuma yako.Ni vipi tutaweza kulijadilia suala hili ikiwa tunaogopa hata kuyatamka maneno haya? |
| 44. | **CIRO** | Ni kweli usemavyo, Cheptoo.!Wajibu wa bunge hili ni kuweka wazi masuala yote yanayogusia haki za Msichana.Sasa ni wapi tena tutaweza kujadilia masuala haya kama si hapa katika bunge hili la wasichana. |
| 45. | **GIRLS** | Nakubaliana nawe!. |

| | | |
|---|---|---|
| 46. | **CHEPTOO** | Nitaufungua mjadala. Fatuma anaona haya kutokana na mabadiliko katika mwili wake.Na swali ni je naweza kufanya ngono nikiwa na umri huu mdogo? |
| 47. | **FATUMA** | Bado naona haya kutoa mchango wangu katika mjadala huu. |
| 48. | **CHEPTOO** | Kwa hivyo hutaki tulijadili suala hili, na tuendelee kufanya makosa au kuchanganyikiwa kama ilivyo sasa? |
| 49. | **CIRO** | Hebu tuendele na mjadala tafadhali. |
| 50. | **FATUMA** | Sawa, na ni kweli najiona nimebadilika kiumbo. Lakini Cheptoo….asizungumzie suala la ngono. |
| 51. | **CIRO** | Kwanini? Yeye ameuliza swali tu? |
| 52. | **FATUMA** | Akiwa na umri wa miaka 15 ni mdogo sana kujihusiana na ngono.Yapasa asubiri. |
| 53. | **CIRO** | Kumbuka mwalimu wa Baiolojia alivyotuambia kuhusu vijana.Alisema homoni ziko kila mahali. |

| | | |
|---|---|---|
| 54. | **ALL** | LAUGHTER |
| 55. | **FATUMA** | Kwa hivyo, tufanye nini kuhusu Cheptoo na suala zima la kufanya mapenzi ndani ya umri alio nao? |
| 56. | **CHEPTOO** | Nadhani nimepata jibu. Nisubiri.Sisi sote bado ni wadogo sana kufanya… inaitwaje vile..eeh kuanza ukware.Lakini hatuwezi kujifanya kwamba hatuyaoni mabadiliko yanayotokea katika mili yetu.Kwa hivyo lazima tujifunze kuhusu mabadiliko haya ili tuweze kujiandaa vyema. |
| 57. | **CIRO** | Cheptoo, Hapo umesema kitu cha maana sana. Tunaweza kutafuta ushauri kutoka kwa walimu wetu.Tusione haya kuwauliza maswali. |
| 58. | **FATUMA** | Pia tujisikie huru kuzungumzia suala hili wazazi. Mnafahamu mabadiliko yote yanayoendelea katika mili yetu. |

59. **CHEPTOO** Sasa,…. Sasa.. nimeshawishika kabisa!. Nitasubiri kidogo kabla ya kuanza kujihusisha na masuala ya ngono. Lakini pia ni lazima tulizungumzia suala hili mara kwa mara. Nimejua kwamba siko peke yangu, nimefurahi sana kwamba tumekuwa na mjadala huu leo.

**60. <u>BRIDGE MUSIC</u>**

**<u>SCENE 4: CIRO'S CLASSROOM. LUNCH HOUR</u>**

**61. SFX: classroom**

62. **CHEPTOO** Ciro… Kumbe uko hapa? Tumekutafuta kila mahali. Hatukutaka kula chakula cha mchana bila kuwa na wewe. Kwani bado unafanya nini darasani?

63. **CIRO** Niacheni peke yangu….! , nendeni zenu!.

64. **FATUMA** Kuna tatizo gani?. Mbona mjeuri hivi?. Tumekuja kukuona kisha,,.

65. **CIRO** nendeni zenu.

66. **CHEPTOO** Hebu inuka Ciro. Nahisi njaa twende tukale.

67. **CIRO** Nimesema siendi, nyinyi nendeni.

| | | |
|---|---|---|
| 68. | **CHEPTOO** | Kuna kitu chakusumbua, sivyo. Hutaki kuinuka kwanini?. |
| 69. | **FATUMA** | Ciro kuna shida gani?. |
| 70. | **CHEPTOO** | Nadhani ni siku zake za hedhi.Tazama alivyochafua sketi yake. |
| 71. | **CIRO** | Nendeni…Naona aibu sana. Wavulana sasa watanichekelea. |
| 72. | **CHEPTOO** | Lakini jambo hili humtokea kila Mwanamke mkamilifu.. Hupasi kuona aibu kwa jambo hili.Sisi sote ni wasichana na hutokea kwa kila mwanamke. |
| 73. | **FATUMA** | Hebu jifunge hiki kitambara changu cha kichwa kisha twende chooni ukajioshe. |
| 74. | **CHEPTOO** | Sisi wasichana tunakumbwa na changamoto nyingi sana maishani. Lazima tuitishe kikao cha bunge letu la wasichana kujadilia suala hili. |
| 75. | **CIRO** | Lakini mnaweza kunisaidia kwanza kabla ya kuwaita wasichana wengine? |

**76. <u>BRIDGE MUSIC</u>**

77. **NARRATOR** Kikao cha bunge kimeitishwa. Wanawake wawili makamu, Janet afisa wa masuala ya Jamii na Mwalimu Mona wamealikwa kuhudhuria kikao hiki na kutoa ushauri wao.

**SCENE 5: GIRLS' PARLIAMENT**

**78. SFX: GIRLS CHATTING (studio)**

79. **CHEPTOO** Kimya kila mmoja. Kama mjuavyo, tumewaalika wasicha wote katika bunge letu. Kwa muongozo wa Mwalimu wetu Mona na Afisa Janet, tunataka kujadilia masuala yanayogusia mili na maumbo yetu. Tujadilie masuala haya yanayowatatiza wengi wasijue la kufanya.

80. **CIRO** Kwanini hatutaji sehemu hizo za mwili tunazo jadilia?

81. **FATUMA** Kwa sababu tunaambia tu ni sehemu za mwili.

82. **CHEPTOO** Lakini haziwezi kuwa vinaya baya kama ni sehemu ya mwili .

| | | |
|---|---|---|
| 83. | **FATUMA** | Siwezi kugusa sehemu zangu za siri. Je Mwalimu Mona hivyo ni vibaya? Nimeambia kwamba ni vibaya je ni kweli.. |
| 84. | **TEACHER MONA** | Sasa ni vipi utaweza kujiosha sehemu hizi? Nataka mujue kitu kimoja. Hakuna sehemu yoyote ya mwili ambayo ni mbaya. Jivunie jinsi ulivyo. Ndio sababu ukaitwa mwanamke. |
| 85. | **CIRO** | Wakati nikiwa katika siku zangu za hedhi, nahisi kuwa ni mchafu sana. Pia naambiwa siwezi kupika kwasababu ni mchafu. Je ni kweli Janet? |
| 86. | **JANET** | Hii ni dhana ambayo ni lazima ibadilishwe. Iwapo Mwanamke hawezi kupata siku zake za hedhi, basi hawawezi kupata watoto, na sasa ulimwengu utakuwa unaelekea wapi? Nyinyi si wachafu, ni wanawake wa kawaida. Mwalimu Mona una jambo la kuongezea? |

| | | |
|---|---|---|
| 87. | **TEACHER MONA** | Bila shaka, ni lazima mujivunie kuwa wanawake. Hata hivyo lakini ni lazima mzingatie kanuni za usafi. Lazima muwe mkibadilisha taulo zenu za hedhi kila baada ya masaa machache ili wavulana wasimuchukulie kuwa ni wachafu. |
| 88. | **FATUMA** | Mara nyingi watu hututania kuhusu mili yetu. Mfano wakati matiti yanapoanza kuota. |
| 89. | **TEACHER MONA** | Watu kama hao wanaomtania au kuwacheka mnapasa kuwapuuza. Wenyewe hawajielewi. |
| 90. | **CIRO** | Mwalimu Mona, ni rahisi kusema kuliko kutenda. Kwanini tusoalke shule nzima kwa shule nzima? |
| 91. | **CHEPTOO** | Au kuima hii nyimbo ambayo nimekuwa nikiiandika na pia kuwafunza wengine. |
| 92. | **CIRO** | Wimbo? |
| 93. | **CHEPTOO** | Ndio, Unaitwa ‘Uwezo wa Msichana’ |
| 94. | **JANET** | Vyema…tufunze basi. |
| 95. | **CHEPTOO** | Sawa tuanze. Imbeni baada ya mimi. |

| | | |
|---|---|---|
| 96. | **NARRATOR** | Na hapo wimbo unatungwa. Wimbo unao jenga imani ya wasichana na kuwakumbusha kwamba wanapasa kujivuna kama Wanawake. Hebu tusikie kama wasicha wote wataweza kuimba wimbo huu uliotungwa na Cheptoo. |
| 97. | **GIRLS** | Sisi ni wasichana, sisi ni wasichana!<br>Tunajivunia kuwa wasichana<br>Tunajivunia mili yetu<br>Mara nyingi huchanganyikiwa kutokana na mabadiliko katika mili yetu Lakini tunafahamu kwamba, haya ni maumbile, kwa hivyo tusiwe na hofu. tusiwe na wasi wasi.<br>Usiogope wala kuona aibu. Usione aibu.<br>Haya ni maumbile na usione aibu.<br>Ni maumbile yanayonifanya kuwa msichana mrembo , mwanamke mrembo.<br>Mwanamke ni kama maua yanayonawiri.<br>Mimi ni msichana na Msichana mrembo.<br>Kwanini nisijivunie kwa jinsi nilivyo?<br>Sisi ni wasichana na tunajivunia kuwa wasichana. |
| 98. | **ALL** | CLAPPING |

| | | |
|---|---|---|
| 99. | **JANET** | Pongezi…pongezi. |
| 100. | **CHEPTOO** | Wimbo mzuri sana. Sisi tumebobea? Lazimea wimbo huu tuwafunze wasichana wote shuleni.. |
| 101. | **CIRO/FATUMA** | Ni lazima! |
| **102.** | **<u>THEME MUSIC</u>** | |

**103. OUTRO**

104. **NARRATOR**

Ni furaha iliyoje kujivunia mili yao na jinsi walivyo. Na wimbo uliotungwa kuwambukusha wa sichanan kwamba ni sharti wajivunie kuwa wasichana na kwamba wajikubali na hali yao ya mabadiliko ya kimaumbile. Katika kipindi kijacho cha Noa Bongo Jenga maisha yako,wasichana hawa watakuwa wakijadilia taaluma wanazoweza kufuatilia. Hivyo usikose kungana nasi usikie mjadala huu kuhusu taaluma za wasichana katika mchezo huu wa haki za wasichana. Pia unaweza kutembea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe kwa maelezo zaidi. Hadi wakati mwengine tutakapoungana tena kwa makala nyingine Kwaheri kwa sasa.